



Tarehe: 05/09//2022

## TANGAZO

### TARATIBU ZA MALIPO YA VIWANJA SAMIA CITY- MJIMWEMA.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani Col. Emanuel Mwaigobeko anapenda kuwatangazia wananchi wote waliopata viwanja vya matumizi mbalimbali katika mradi wa Upimaji Viwanja Mjimwema “**SAMIA CITY**” kuwa wanatakiwa kufika Ofisi ya ardhi (**CENTRE**) kuchukua ankara za malipo na kufanya malipo yote au nusu ya gharama ya malipo ya viwanja walivyopewa.

Malipo ya awali (malipo ya nusu ya gharama ya kiwanja) yanatakiwa kufanyika kupitia benki ya **NMB NO. 70610000863 MTR MUN COUNCIL MISCELLANEOUS ACCOUNT** ndani ya siku kumi na nne tangu orodha ya majina ya waliopata viwanja ilipotolewa **tarehe 30.08.2022** na baada ya miezi mitatu malipo yote yanatakiwa kuwa yameshakamilika.

Orodha ya Majina ya waombaji waliopata Viwanja imebandikwa kwenye mbao za matangazo za Ofisi za Kata, Ofisi za ardhi, Ofisi za Manispaa, sehemu zenye mikusanyiko ya watu wengi kama (Stendi ya mabasi Nkanaredi na kwenye Tovuti ya Manispaa [www.mtwaramikindanimc.go.tz](http://www.mtwaramikindanimc.go.tz)

Endapo malipo hayo hayatakamilishwa kwa wakati, malipo yaliyotangulizwa hayatarejeshwa na kiwanja kitagawiwa kwa mwombaji mwingine bila kutoa taarifa yoyote kwako.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na namba ya simu **0714 538 282**.

Limetolewa na:-

**OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA  
MTWARA-MIKINDANI**